# MAENEO/VIFUNGU VINAVYOHITAJI KUFANYIWA MAREKEBISHO KWENYE SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI.

## HOJA INAYOHITAJI KUREKEBISHWA

1. Baadhi ya Sheria Ndogo za Halmashauri zinatoa adhabu kwa mkosaji kulipa faini **ya** Shilingi 300,000/= ambayo inakinzana na Sheria Mama (Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 Toleo la 2002 inayosema faini isiyozidi shilingi 300,000/=

**Agizo**

Vifungu vya Sheria Ndogo zote za Halmashauri zenye kasoro kama hizi zirekebishwe ili kuweka adhabu ya faini **isiyozidi** shilingi laki tatu (300,000/=) .

2. Baadhi ya Sheria Ndogo zinazohusu Hifadhi ya Mazingira na Usafi wa Mazingira zimeweka Ada ya Taka bila kuainisha muda maalum wa kulipa ada ya taka kama ni kwa mwaka au mwezi na baadhi ya Ada zinazotozwa ni kubwa kwa baadhi ya wazalishaji wa taka hizo, mfano wasambazaji wa magazeti, vocha na maji ya kunywa.

**Agizo**

Sheria Ndogo zenye kasoro hizi zirekebishwe kwa kuainisha muda wa kulipa ada ya taka, mfano Sheria Ndogo inaweza kusema ada italipwa kwa siku, mwezi, au mwaka. Pia viwango vya ada ya Taka vilivyoorodheshwa kwenye Sheria Ndogo hizo virekebishwe kwa kuweka viwango stahiki kwa kila aina ya mzalishaji taka na ionyeshe viwango visivyoleta kero kwa wananchi.

3. Baadhi ya Sheria Ndogo hazijaonyesha mamlaka inayohusika na kuidhinishwa kwa Sheria Ndogo. Haya ni makosa ya uchapishaji, hivyo Sheria Ndogo yenye kasoro kama hili inakosa uhalali wa kutumika na ni kinyume na Kifungu cha 36(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1;

**Agizo**

Sheria Ndogo zenye kasoro kama hii zirekebishwe kwa kuonyesha zimetungwa chini ya mamlaka ipi na kwa mujibu wa Sheria ipi na kifungu kipi cha Sheria mama (Sheria ya Serikali za Mitaa).

4. Baadhi ya Sheria Ndogo hazijaweka wajibu kwa Halmashauri wa kulipa fidia ya hasara itakayosababishwa na Afisa mwidhiniwa au afisa yeyote ama kwa uzembe au kwa maksudi wakati wa kukusanya Ada au ushuru au wakati anatekeleza Sheria Ndogo za Halmashauri.

**Agizo**
Vifungu vya Sheria Ndogo zote ambavyo havitoi wajibu kwa Halmashauri kulipa fidia kwa hasara itakayosababishwa na Afisa mwidhiniwa wakati anatekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi, virekebishwe ili kutoa wajibu huo wa Halmashauri wa kulipa fidia. Hali hii itaifanya Halmashauri kuwa makini wakati wa kutekeleza majukumu yake.

5. Baadhi ya Sheria Ndogo za Halmashauri zimeweka adhabu ya kifungo cha juu kuliko kilichowekwa chini ya kifungu cha 36(i) cha Sheria ya fedha za Serikali za Mitaa sura 290

**Agizo**
Vifungu vya Sheria Ndogo zote za Halmashauri zenye kasoro hii zirekebishwe ili kuweka adhabu ya kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) kama inavyoelezwa kwenye kifungu cha 36(i) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa sura 290.

6. Baadhi ya Sheria Ndogo za Halmashauri zimeweka kifungu kinachomlazimisha mkosaji kukiri kosa na kujaza fomu maalum kinyume cha Sheria mama ambayo haijaweka ulazima wa mkosaji kukiri kosa.Sheria inataka mkosaji akiri kwa hiari yake mwenyewe

**Agizo**
Vifungu vya Sheria Ndogo zenye kasoro hii virekebishwe kwa kuweka uhiari wa mkosaji kukiri kosa kabla ya kufikishwa mahakamani (kufifirisha kosa) kwani ni Mahakama pekee ndiyo yenye Mamlaka ya kumtia hatiani mtuhumiwa.

7. Baadhi ya Sheria Ndogo za Halmashauri zinatoa tafsiri ya maneno mbalimbali yasiyokidhi maana halisi na hivyo kuwa na wigo mdogo wa uelewa na kuwa kero wakati wa kutekeleza Sheria husika. Mfano tafsiri ya neno mnyama mazao n.k

**Agizo**
Sheria Ndogo zenye kasoro hizi zirekebishwe kwa kuwa na tafsiri yenye wigo mpana, kwa kutumia tafsiri ya neno husika kutoka kwenye Sheria mama

8. Baadhi ya Sheria Ndogo za Halmashauri zimeweka faini **isiyopungua** shs. 50,000/- ambayo ni kinyume na masharti ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa mayoeleza adhabu ya faini **isiyozidi** shs. 50,000/=

"Diwani au mtu yeyote atakayekiuka vipengele vya Kanuni hizi atahesabika ametenda kosa chini ya Kifungu cha 65(4) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288 Toleo la 2002 na Kifungu cha 120(4) cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 Toleo la 2002, na atastahili kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Kifungu cha 96 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura 16 Toleo la 2002.

13. Kanuni za Kudumu zina Kifungu kinachompa haki mjumbe wa Halmashauri (Diwani) ya kupata waraka wowote uliojadiliwa na Kamati ya Halmashauri. Hata hivyo Kanuni inaweka masharti kuwa atapata waraka huo **"Kama nakala itapatikana"** masharti haya yanakinzana na maudhui ya upatikanaji wa taarifa.

**Agizo**

Kanuni za Kudumu zenye kasoro hii zirekebishwe kwa kuondoa maneno **"kama nakala zinapatikana"** ili haki ya kupata nakala iweze kutendeka na pia kutoa uhakika wa kupatikana kwa nakala hizo kwa kuwa ni haki kwa mjumbe kupewa nakala pale anapohitaji.

14. Baadhi ya Kanuni za Kudumu za Halmashauri zinampa uwezo Mwenyekiti / Meya wa Halmashauri wa kuamua juu ya jambo lolote wakati wa vikao vya Halmashauri, lakini hazitoi haki kwa mjumbe ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mwenyekiti / Meya ili kumuwezesha kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo.

**Agizo**

Kanuni za Kudumu zirekebishwe na kuweka utaratibu kama unaotumika na Bunge kuhusu maamuzi ya Spika wa Bunge kwa kutoa haki kwa mjumbe ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mwenyekiti /Meya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo kwenye Kamati ya Rufaa. Kanuni iweke utaratibu wa Diwani ambaye hakuridhika kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufaa, na inapendekezwa Kamati ya Maadili ipewe jukumu hilo la kusikiliza na kutolea uamuzi rufaa hizo.

15. Baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikinakili neno kwa neno (copying and pasting) Sheria Ndogo kutoka katika Halmashauri nyingine bila ya kufanya marekebisho ya msingi na kusababisha kunakili dosari za Sheria Ndogo hizo. Mfano Sheria ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira kwa Halmashauri za Wilaya zimekuwa zikinakili Sheria Ndogo hiyo kutoka kwenye Halmashauri za Miji na kuweka marufuku ya kupanda mimea mirefu wakati marufuku kama hii inafaa zaidi Mijini.

**Agizo**

Halmashauri zipitie Sheria Ndogo zake zote ili kurekebisha kasoro zinazotokana na kunakili Sheria Ndogo zenye maudhui tofauti na hali ya mazingira ya Halmashauri husika

**Agizo**

Sheria Ndogo zenye kasoro hizi zirekebishwe ili kuendana na matakwa ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa sura 290

9. Kanuni za Kudumu za uendeshaji wa Halmashauri zina kifungu kinachozungumzia mazingira ambapo mjumbe anaweza kuadhibiwa kwa kutoa kauli zenye kashfa dhidi ya mtu yoyote, hata hivyo Kanuni hii haijaweka wazi kuwa kauli zenye kashfa ni zipi.

**Agizo**

Kanuni za Halmashauri zenye kasoro hii zirekebishwe kwa kutoa tafsiri ya neno "**Kauli zenye kashfa**" ili kuweka bayana kauli zinazoweza kuchukuliwa kuwa ni kauli zenye kashfa na hivyo kuwa wazi na kueleweka kwa wajumbe wote badala ya kuacha mwenyekiti kuamua kama kauli hiyo ni yenye kashfa au laa.

10. Kanuni za Kudumu za uendeshaji wa Halmashauri zina kifungu cha Kanuni kinachoelezea adhabu inayoweza kutolewa kwa mjumbe ni kumtolea haki zote ikiwa ni pamoja na kinga, posho na upendeleo. Adhabu hii inakiuka misingi ya Sheria.

**Agizo**

Kanuni za Kudumu za Halmashauri zenye Kanuni kama hiyo irekebishwe kwa kuondoa maneno "Upendeleo na Kinga" ili kumpa haki mjumbe ya kuwa na kinga.

11. Kanuni za Kudumu zinaelezea kuhusu Kanuni ya uvunjaji wa mkataba, lakini Kanuni hii haiko wazi kwa kuwa haitaji masharti gani yanapaswa kuzingatiwa ili Mkataba uweze kuvunjwa kama Sheria ya Mikataba Sura 345 toleo la 2002 inavyobainisha.

**Agizo**

Kanuni za Kudumu zenye kasoro hiyo, zirekebishwe kwa kufanya marekebisho kwenye Kanuni hiyo kwa kuongeza masharti yaliyowekwa kwenye Sheria ya Mikataba Sura 345 Toleo la 2002 kuhusu masharti ya kuvunja mkataba.

12. Kanuni za Kudumu zina Kanuni inayoainisha masuala kadhaa kuhusu Diwani kutokuwa na maslahi binafsi katika Mikataba inayoingiwa na Halmashauri juu ya utoaji wa Huduma mbalimbali. Kanuni hiyo inamtaka Diwani kubainisha maslahi yake waziwazi lakini haijaweka adhabu au hatua inayopaswa kuchukuliwa pale ambapo Diwani akigundulika hakuweka wazi maslahi aliyokuwa nayo katika Mkataba wowote ulioingiwa na Halmashauri na yeye kuwa na maslahi nayo.

**Agizo**

Kanuni ya Kudumu yenye kasoro hii ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza Kanuni Ndogo kwenye Kanuni hiyo itakayosomeka kama ifuatavyo: